# OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

# WIKI HII KWENYE MAGAZETI NA MITANDAO


14/10/2024 ► 18/10/2024

OAG

OFISI YA RAIS TAMISEMI
JIANDIKISHE PIGA KURA
27 NOVEMBA 2024
UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA

## MOTISHA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Profesa Palamagamba Kabudi (kushoto), akimkabidhi Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Jaji mstaafu Mathew Mwaimukiasi, sh. milioni sita kutekeleza ahadi iliyotolewa na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Charles Maswi (wa pili kushoto), zikiwa motisha kwa watumishi wawili waliofanya kazi katika tume hiyo kwa zaidi ya miaka 30, wizarani hapo jijini Dodoma, mwishoni mwa wiki. (Picha na Wizara ya Katiba na Sheria).



# AG ataka watumishi, mawakili kujiandikisha daftari la wapigakura

Na Anastazia Anyimike

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali, Hamza Johari amejiandikisha katika Orodha ya Wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa huku akiwataka watumishi wa ofisi yake na mawakili wote kwenda kujiandikisha.

Akizungumza baada ya kujiandikisha katika kituo cha Mbuyuni Kata ya Ipagala, Wilaya ya Dodoma Mjini mkoani Dodoma, Johari alisema ni vyema watumishi wa ofisi yake na mawakili kote nchini kutumia siku zilizobaki kwenda kujiandikisha.

"Napenda kuwapa hamasa na kuwahamasisha watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakikisha wanatumia vizuri haki yao ya kikatiba ya kupigakura itakapofika Novemba 27, mwaka huu kwa ajili ya kuwachagua viongozi wetu wa serikali za mitaa.

"Lakini haki hiyo inaanza na wajibu wa wewe kama mtumishi kujiandikisha katika orodha ya wapigakura. Mimi kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali leo (juzi) nimejiandikisha hapa katika kituo cha Mbuyuni Kata ya Ipagala eneo ambalo ndio eneo ninaloishi," alisema.

Johari alisema anajua tayari kuna ambao wamejiandikisha na kusisitiza kuwa kwa wale ambao bado wahakikishe wanakwenda kujiandikisha kabla au ifikapo Oktoba 20, mwaka huu.

Utaratibu wa kuandikisha wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa uliopangwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu umeanza Oktoba 11 hadi 20, mwaka huu.

Scanned with CamScanner

OFISI YA RAIS TAMISEMI
JIANDIKISHE PIGA KURA
27 NOVEMBA 2024
UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA

FULLSHANGWE blog
CONTACT:
phone: +255 713 410 676
+255 755 333 372
P.O BOX 78392, Dar es Salaam
Email. johnbukuku@gmail.com

Home Biashara Burudani Magazeti Mchanganyiko Michezo Siasa Teknolojia TV Makala

UNCATEGORIZED

# MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AJIANDIKISHA KWENYE DAFTARI LA MPIGA KURA

John Bukuku | 2 days ago
Last updated: 2024/10/16 at 5:36 PM

Share



Home Jiachie Blog Mtaa Kwa Mtaa Blog MK Computer Tweaks

Michuzi Blog | MICHUZI TV

This Space can Only be yours Call us today on +255 754 271 266

Habari Biashara Kimataifa Burudani Michezo Magazeti Zanzibar Michuzi TV Contact Us Zilizobamba

# MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AJIANDIKISHA KWENYE DAFTARI LA MPIGA KURA

MICHUZI BLOG AT WEDNESDAY, OCTOBER 16, 2024 HABARI,

Na Mwandishi wetu- Dodoma

Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza Johari tarehe 16 Oktoba 2024 amejiandikisha, kwenye Daftari la Mpiga Kura katika Kata ya Ipagala Kituo cha Mbuyuni, Ilazo Jijini Dodoma ikiwa ni hatua kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 unaotarajia kufanyika Novemba 27 Mwaka huu.

Akizungumza mara baada ya kujiandikisha kwenye kituo hicho Mwanasheria Mkuu wa Serikali alitumia fursa hiyo kuwahamasisha Watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kujiandikisha katika Daftari la Mpiga Kura ili kutimiza haki yao ya msingi ya Kikatiba ya kupiga kura katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu.

"Nachukua nafasi hii kuwahamasisha Watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakikisha kwamba wanatumia haki yao vizuri ya kikatiba ya kupiga kura itakapofika tarehe 27 Novemba 2024 kwa ajili ya kuwachagua Viongozi wetu wa Serikali za Mitaa".

Aidha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali amewakumbusha Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutimiza wajibu wa kujiandikisha kwenye Daftari la Mpiga Kura ili waweze kupata haki ya kushiriki kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

OFISI YA RAIS TAMISEMI JIANDIKISHE PIGA KURA 27 NOVEMBA 2024 UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA

Home About Us Privacy Policy Contact Us

DIRAMAKINI ARTICLES LOCAL NEWS INTER NEWS ADVERTS NEWSPAPERS PHOTO EVENTS

Home > Habari

FOLLOW US

# Mwanasheria Mkuu wa Serikali ajiandikisha kwenye Daftari la Mpiga Kura

**DODOMA-Mwanasheria Mkuu** wa Serikali Mhe. Hamza Johari tarehe 16 Oktoba 2024 amejiandikisha, kwenye Daftari la Mpiga Kura katika Kata ya Ipagala Kituo cha Mbuyuni, Ilazo jijini Dodoma ikiwa ni hatua kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 unaotarajia kufanyika Novemba 27, mwaka huu.



OFISI YA RAIS TAMISEMI
JIANDIKISHE PIGA KURA
27 NOVEMBA 2024
UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA

oagtanzania



View insights

Boost post

33 likes

oagtanzania MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AJIANDIKISHA KWENYE DAFTARI LA MPIGA KURA

**Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**
@Oag_tz




23:45 · 16 Oct 24 · **1** View

# TUPO KARIBU YAKO!

## Tufuatilie kupitia

oagtanzania

info@oag.go.tz

www.oag.go.tz

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
Mtaa wa Mtumishi
Mji wa Serikali Mtumba
S. L. P 630
Dodoma - Tanzania

**KWA MSAADA WA HUDUMA ZA KISHERIA PIGA SIMU BURE 0800 11 0188**

Weledi na Ubora